LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# USHAHIDI

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# USHAHIDI

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO

**SHUKRANI** ........ **5**
**1. UTANGULIZI** ........ **8**
**2. MAANA YA USHAHIDI** ........ **8**
2.1.Aina za Ushahidi ........ 8
2.1.1.Ushahidi wa Matamshi ........ 9
2.1.2.Ushahidi wa Maandishi ........ 9
2.1.3.Ushahidi Halisia ........ 10
2.1.4.Ushahidi wa Kimazingira ........ 10
**3. KUTHIBITISHA TUHUMA, MASHTAKA, SHAURI AU USHAHIDI MAHAKAMANI** ........ **11**
**4. KUKANUSHA TUHUMA, MASHTAKA, SHAURI AU USHAHIDI MAHAKAMANI** ........ **11**
**5. AINA ZA MASHAHIDI** ........ **12**
5.1.Shahidi ni Nani? ........ 12
5.2.Nani Anaweza kuwa Shahidi? ........ 12
5.3.Mume na Mke ........ 13
5.4.Shahidi wa Utaalamu Maalum au Fani ........ 14
5.5.Mtu mwenye Matatizo ya Akili (Mwenye Mtindio wa Ubongo) ........ 14
**6. KUHOJI NA KUULIZA MASWALI MASHAHIDI** ........ **15**
6.1.Upande wa Mashtaka au Mlalamikaji ........ 15
6.2.Upande wa Utetezi au Mdaiwa ........ 16
6.3.Mahakama ........ 16
**7. KUPOKELEWA NA KUKUBALIWA KWA USHAHIDI MAHAKAMANI** ........ **17**
**8. HITIMISHO** ........ **17**

## SHUKRANI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapenda kutoa shukrani kwa wanasheria wake wote, wakiwemo wale wa kujitolea, walioshiriki katika uandaaji wa kijarida hiki. Pia, Kituo kinawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki katika kuandaa toleo hili la nne la kukirejea kijarida hiki, husussan Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Bi. Irene Nambuo na Bw. Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kwamba kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zote, na hata baadhi ya sheria

zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Ni matarajio yetu kwamba utasoma kijarida hiki kwa makini; na pale ambapo suala lako litakwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi tafuta msaada wa kisheria au nenda kwa mwanasheria yeyote aliye karibu nawe kwa msaada zaidi.

Ni matarajio yetu kwamba utasoma kijarida hiki kwa makini; na pale ambapo suala lako litakwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi tafuta msaada wa kisheria au nenda kwa mwanasheria yeyote aliye karibu nawe kwa msaada zaidi.

Tunaamini kijarida hiki kitakusaidia kupata maelezo muhimu kuhusu ushahidi nchini Tanzania. Tafadhali, umalizapo kusoma kijarida hiki mjuze na mwenzako au mpatie naye akisome na kupata maarifa.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiaa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama shirika lisilo la kiserikali, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Kijitonyama, jijini Dar es Salaam. Kituo pia kina ofisi nyingine ndogo mbili, ambazo ni Ofisi ya Kinondoni – Dar es Salaam, ambayo imejikita katika kutoa msaada wa kisheria; na Ofisi iliyopo Sakina, jijini Arusha.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kupitia njia ya utoaji elimu na msaada wa kisheria.

# 1. UTANGULIZI

Masuala yanayohusu ushahidi nchini yanasimamiwa na Sheria ya Ushahidi, ya mwaka 1967, Sura ya 6 ya Sheria za Tanzania, mapitio ya mwaka, 2002. Sheria hii inaweka masharti ya jumla ya sheria ya ushahidi nchini Tanzania; japo sheria nyingine zinaweza pia kuweka vipengele maalum kuhusiana na mazingira na mahitaji maalum ya sheria husika.

# 2. MAANA YA USHAHIDI

Ushahidi ni njia ambayo hutumika kuthibitisha au kukanusha masuala au tuhuma iliyopo au jambo linalobishaniwa.

## 2.1. Aina za Ushahidi

Kuna aina kuu nne za ushahidi nazo ni:-

1. Ushahidi wa matamshi;
2. Ushahidi wa maandishi;
3. Ushahidi wa uhalisia; na
4. Ushahidi wa kimazingira.

### 2.1.1. Ushahidi wa Matamshi

Huu ni ushahidi usio wa maandishi ambao hutolewa moja kwa moja kupitia mdomo wa shahidi. Misingi ya kukubalika ushahidi huu ni kama ifuatavyo:-

a. Iwapo unahusisha suala la kuona, ushahidi huo unatolewa na shahidi aliyeshuhudia kuona kitendo hicho;
b. Iwapo unahusisha kusikia, ni lazima utolewe na shahidi aliyesikia;
c. Iwapo unahusisha hisia nyinginezo tofauti na kusikia pamoja na kuona ni lazima ushahidi huo utolewe na shahidi aliyepata hisia hizo mfano, kuguswa, kuonja au kunusa.

### 2.1.2. Ushahidi wa Maandishi

Ushahidi wa maandishi ni ushahidi wowote unaotolewa kwa maandishi mahakamani. Ushahidi huu unaweza kuwa katika nyaraka, picha, alama yoyote, kanda ya video/kaseti au redio au katika hali yoyote, ambayo ni imara,

ya kudumu na kusomeka au kutambulika.

Ushahidi wa maandishi unatakiwa uwe katika hali ya asilia (original) isipokuwa pale sheria inaporuhusu unaweza kutolewa kwa nakala (copies).

### 2.1.3. Ushahidi Halisia

Ushahidi wa uhalisia, ni ushahidi ambao unatolewa kwa kuonyesha kitu, mfano kisu kilichotumika kuua, au mikanda ya video, au picha, au kutembelea eneo la tukio, mfano pale panapotokea mgogoro wa shamba.

### 2.1.4. Ushahidi wa Kimazingira

Ushahidi wa kimazingira ni ushahidi unaopatikana baada ya kuunganisha matukio, sehemu tukio lilipotokea na maelezo yanayotoa tafsiri ya mazingira maalum yanayothibitisha jambo au tukio.

## 3. KUTHIBITISHA TUHUMA, MASHTAKA, SHAURI AU USHAHIDI MAHAKAMANI

Mtu yeyote ambaye anashtaki, amefungua shauri, anaiomba au kuitaka mahakama itoe uamuzi au hukumu katika mashtaka au shauri kwa manufaa yake, analazimika kuwasilisha mahakamani ushahidi unaojenga hoja kuthibitisha madai au tuhuma anazozitoa dhidi ya mtuhumiwa, mshtakiwa au mdaiwa. Kiwango cha uthibitishaji wa tuhuma, dai au hoja katika kesi ya jinai ni kutokuacha shaka yoyote; na katika kesi ya daawa ni ukweli kwa kiwango kikubwa au cha kusadikika.

## 4. KUKANUSHA TUHUMA, MASHTAKA, SHAURI AU USHAHIDI MAHAKAMANI

Ni wajibu wa mtu yeyote ambaye anatuhumiwa, anashtakiwa au ushahidi umetolewa dhidi yake katika shauri kujitetea, kukanusha tuhuma, shtaka au ushahidi uliotolewa dhidi yake, kwani asipofanya hivyo mahakama inaweza kutoa uamuzi dhidi yake.

# 5. AINA ZA MASHAHIDI

## 5.1. Shahidi ni Nani?

Shahidi ni mtu yeyote ambaye anatoa maelezo kuthibitisha tuhuma, shtaka au tukio fulani mbele ya mahakama.

## 5.2. Nani Anaweza kuwa Shahidi?

Kutokana na Sheria ya Ushahidi ya mwaka 1967, watu wote wanaweza kuwa mashahidi isipokuwa pale Mahakama itakapoona kuwa hawaelewi kile wanachokisema au kuulizwa na pia hawatoi majibu ya kueleweka, labda kwa sababu ya umri mdogo, uzee, magonjwa au kitu kingine chochote.

Mfano; mtoto mdogo wa chini ya umri wa miaka (14) anaweza kutoa ushahidi juu ya jambo fulani na ushahidi wake ukapokelewa kwa kiapo, ikiwa mtoto huyo ataonekana kuelewa maana ya kiapo. Ikiwa mahakama itaona mtoto haelewi maana ya kiapo, ushahidi wake utachukuliwa kwa kuangalia kuwa mtoto ni muelewa na anaelewa kwamba anatakiwa kuongea ukweli mtupu

mbele ya mahakama.

Kwa kawaida, mahakama inatakiwa kujitahadharisha yenyewe wakati inapopokea na kutumia ushahidi wa mtoto.

### 5.3. Mume na Mke

Sheria inaeleza kuwa mume au mke ni mashahidi ambao wanaweza kutoa ushahidi lakini kila mmoja hawezi kulazimishwa kutoa ushahidi dhidi ya mwenzi wake, isipokuwa kwenye mashtaka yanayohusu makosa ya kujamiiana na yaliyo kwenye sheria ya ndoa au kama kosa analoshitakiwa nalo linamhusu mke, mume, mtoto au mali zao.

Mwendesha mashtaka anaweza kumuita mume au mke kama shahidi wake kwa namna yoyote ile, mfano kwa maandishi au kutoa ishara, ili mradi ushahidi wake ueleweke; na ni lazima ushahidi huo utolewe katika Mahakama ya wazi. Ushahidi wa aina hii unachukuliwa kama ushahidi wa matamshi.

### 5.4. Shahidi wa Utaalamu Maalum au Fani

Ushahidi wa mtaalamu juu ya jambo fulani pia hukubalika. Mfano, daktari anaweza kutoa ushahidi kuhusu sababu ya kifo cha mtu ambaye alimtibu au kufanya uchunguzi wa sababu ya kifo chake.

### 5.5. Mtu mwenye Matatizo ya Akili (Mwenye Mtindio wa Ubongo)

Mtu mwenye matatizo ya akili anaweza kutoa ushahidi kwa kitu anachokielewa isipokuwa pale mahakama itakapoona kwamba haelewi anachosema au kuulizwa na hivyo ushahidi wake kutokuaminika na hajui maana ya kiapo.

Muhimu

Mahakama haifungwi na ushahidi wa utaalamu maalum au fani; bali inaupima kama ushahidi mwingine na inaweza kuukataa au kutouzingatia katika kutoa maamuzi yake.

# 6. KUHOJI NA KUULIZA MASWALI MASHAHIDI

Shahidi anayetoa ushahidi mbele ya Mahakama anaulizwa maswali na pande tatu;

i. Upande wa mashtaka, mdai au mlalamikaji anaouunga mkono katika ushahidi;
ii. Upande wa utetezi, mlalamikiwa au mdaiwa;
iii. Mahakama.

## 6.1. Upande wa Mashtaka au Mlalamikaji

Mtu yoyote ambaye analalamika au kushtaki, ana haki ya kuita mashahidi ambao atawauliza maswali kwa lengo la kuthibitisha madai au mashtaka yake. Mashahidi hawa wanatakiwa kuunga mkono yale anayoyasema/anayolalamikia ili kuweza kuyathibitisha na hivyo kuweza kujenga kesi au shauri lake na hatimaye kushinda.

Maswali anayotakiwa kuwauliza mashahidi wake yasiwe ya kuwaongoza, bali ya kuwawezesha kueleza ukweli wanaofahamu kuhusu jambo linalobishaniwa. Upande wa mdaiwa/mshitakiwa una haki ya kuwauliza maswali mashahidi wa upande wa utetezi kwa lengo la kudhoofisha,

kukanusha au kupima ukweli na uzito wa ushahidi uliotolewa na mdai au mshitaki.

### 6.2. Upande wa Utetezi au Mdaiwa

Upande wa utetezi au mdaiwa una haki ya kuita mashahidi wake na kuwauliza maswali kwa lengo la kujenga utetezi wake. Maswali hayo yasiwe ya kumuongoza shahidi kusema mambo ambayo mdaiwa anataka aseme. Ushahidi uwe ni wa kujenga kesi ya utetezi kwa kueleza ukweli unaomwondolea mdaiwa/mshitakiwa hatia au lawama.

Vile vile upande wa mdai au mshitaki una haki ya kuwauliza mashahidi wa mdaiwa/mshitakiwa maswali kwa lengo la kukanusha, kudhoofisha au kupima ukweli na uzito wa ushahidi uliotolewa na upande wa mdaiwa/mshitakiwa.

### 6.3. Mahakama

Mahakama ina haki ya kuuliza maswali pande zote katika shtaka au shauri ili kupata ufafanuzi au ukweli wa jambo linalobishaniwa.

## 7. KUPOKELEWA NA KUKUBALIWA KWA USHAHIDI MAHAKAMANI

Mahakama ndiyo yenye mamlaka ya kukubali au kukataa kupokea ushahidi. Mahakama inafanya hivyo kwa kuzingatia kanuni za utoaji ushahidi na kama ushahidi huo unahusu suala linalobishaniwa.

## 8. HITIMISHO

Ni muhimu kuzingatia na kufuata kanuni za utoaji ushahidi ili ushahidi ukubalike mahakamani kwa ajili ya kukanusha au kuthibitisha jambo linalobishaniwa, ili mtu aweze kupata haki yake.

Mashahidi wa upande mmoja, mfano mdai, mshtaki au mlalamikaji wanatakiwa kutoa ushahidi unaoshabihiana (ambao haupingani), ili kuweza kuthibitisha jambo linalobishaniwa. Vilevile, kwa upande wa utetezi inapaswa kuwa vivyo hivyo.

Idadi ya mashahidi si hoja bali kinachotakiwa ni ukweli, uzito na kushabihiana kwa ushahidi unaotolewa. Hivyo shahidi mmoja anaweza kuwa na ushahidi mzuri na

kuthibitisha jambo linalobishaniwa vizuri zaidi kuliko mashahidi wengi ambao hawajui wayasemayo na ushahidi wao unapingana au hauna mtiririko mzuri. Hivyo, kabla mtu hajafungua shauri au mashtaka mahakamani, ni vyema ajiulize kama ana ushahidi wa kutosha au la; na kabla hajajitetea au kukanusha mashtaka, tuhuma au madai dhidi yake, ni vyema ajiulize kama ana ushahidi wa kutosha.

Ndugu msomaji, umepata elimu ya kutosha kuhusu ushahidi, pamoja na kanuni za utoaji ushahidi mahakamani. Ombi letu ni kwamba elimu hii uliyoipata usikae nayo mwenyewe, bali uitoe kwa wanajamii wengine ili tuweze kujenga jamii yenye ufahamu wa kutosha kuhusu sheria za nchi, ikiwemo sheria inayohusu ushahidi.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*